

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Anuani ya Simu "TAMISEMI" DODOMA

Simu Na: +255 26 2321607

Nukushi: +255 26 2322116

Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:-



Mji wa Serikali – Mtumba,
Mtaa wa TAMISEMI,
S.L.P. 1923,
41185 DODOMA.

Kumb. Na. DB.121/297/03/65


10 Januari, 2022

Makatibu Tawala wa Mikoa,
TANZANIA BARA.

Yah: **MATUMIZI YA KALENDA ZA UTEKELEZAJI WA MITAALA YA ELIMU YA AWALI, MSINGI NA SEKONDARI**

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu

2. Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Tenknolojia wameandaa miongozo na kalenda za utekelezaji wa mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari. Malengo ya kalenda hizo ni kuimarisha usimamizi wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwa kuleta ulinganifu wa kile kinachofundishwa katika Shule zote za Msingi na Sekondari nchini. Aidha, kalenda hizo zitasaidia:
 - a) Kumwongoza mwalimu kuandaa Azimio la Kazi na Andalio la Somo kwa kuzingatia muda na idadi ya vipindi vilivyoelekezwa katika kalenda;
 - b) Kumwongoza mwalimu kuwawezesha wanafunzi kukuza umahiri uliobainishwa kwenye mtaala kwa kuzingatia muda ulioelekezwa katika kalenda;
 - c) Kumwongoza mwalimu kufanya upimaji wa ujifunzaji kwa kuzingatia maudhui yaliyoelekezwa kufundishwa katika kalenda ya mwaka;
 - d) Kuwaongoza wasimamizi wa utekelezaji wa mtaala na Wathibiti Ubora wa Shule kufanya ufuatiliaji na tathmini ya ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji shuleni; na
 - e) Kuwaongoza wapimaji na watahini kuandaa mitihani inayoendana na mtiririko wa ujifunzaji.
3. Kalenda za utekelezaji wa mitaala zinaanza kutumia mwaka masomo unaoanza tarehe 17 Januari 2022. Kwa barua hii, waelekeze Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa watoe maelekezo kwa Maafisa Elimu Kata, Wakuu wa Shule na walimu wa Shule za Msingi na Sekondari kuandaa mipango ya ufundishaji (Maazimio ya Kazi) kwa mwaka 2022 kwa kuzingatia kalenda hizo. Sekretarieti za Mikoa ziwasilishe taarifa ya utekelezaji wa kalenda za utekelezaji wa mitaala kila robo mwaka wa masomo.
4. Pamoja na barua hii, nimeambatisha kalenda za utekelezaji wa mitaala kwa mwaka wa masomo 2022 ambazo pia zinapatikana kupitia www.tamisemi.go.tz kwa utekelezaji.
5. Ninakutakia utekelezaji mwema.


Prof. Riziki S. Shemdoe
KATIBU MKUU